

Utunzaji na uhifadhi wa nafaka ya mahindi

UTANGULIZI

Asilimia 80 ya mahindi yanayovunwa nchini huhifadhiwa kwenye ghala za nyumbani, Kati ya asilimia 20 hadi 30 ya mavuno hupotea katika miezi 6 iwapo hakuna hatua za kuzuia zinazochukuliwa. Hasara kubwa ni kutokana na wadudu, panya na magonjwa. Wadudu wa mahindi yaliyowekwa ghalani ni

- . Wadudu walao mahindi
- . Wadudu wanaotoba nafaka "scania"
- . Nondo na mende

Panya wa nyumba na vichaka

Magonjwa ya kuota kuvu na ukungu

HATUA ZA KUKINGA UHARIBIFU NI

Kuvuna kwa wakati ufaao

- . Uvunaji ufanywe mahindi kavu yainamapo
- Kukausha vizuri
- . Uvunaji wa mikono ufuatwe na ukaushaji kwenye sehemu zilizoinuliwa au hema zilizotandikwa
- . Hori zilizo wazi au vikapu vyenye mashimo, baadae mahindi yabambuliwe na yatiwe dawa

USAIFI WA GHALA

- . Maghala yasafishwe ili kuondoa nafaka za awali
- . Dawa ipulizwe ili kuua wadudu wowote

KUZITIBU NAFAKA

Nafaka ziwekwe dawa ya vumbi ya kuhifadhi kwa kiasi cha gramu 50 kwa kila kilo 90 zinazopatikana katka maduka ya kuuza madawa ya kilimo

- . Kifaa cha kupimia kiwango hiki kimefungwa pamoja na dawa
- . Nafaka ziwekwe kwenye mikeka na kuchanganywa vizuri na dawa ya vumbi kwa kutumia koleo

- . Kibonge cha sufi pia chaweza kutumika kuchanganya nafaka
- . Kuanika juu pia husaidia kuondoa wadudu lakini ni lazima mtindo huu ufanikishwe kwa kuongezea dawa
- . Panya wadhibitiwe kwa kutumia paka, mitego au chambo

HOJA ZA KUKUMBUKA

- . Sharti mahindi yakauke kabisa ili kuzuia kushambuliwa na ukungu
- . Mahindi yanye kiwango kikubwa cha unyevu hupunguza ufanisi wa dawa
- . Mahindi yanapobambuliwa yatiwe dawa na kuhifadhiwa katika magunia au vifaa vingine vigumu kama mapipa
- . Hamisha magunia haya hadi kwenye ghala na wakinge panya
- . Ikiwa yamehifadhiwa ndani ya nyumba tumia sehemu iliyoinuliwa au kwenye visiki ili kuzuia kuota kuvu
- . Tenga nafasi kutoka kwenye ukuta ili kuwezesha kukagua vizuri
- . Tia dawa tene baada ya miezi 6

KWA MAWASILIANO ZAIDI

Emmanuel Mabula

Mtaalamu wa kilimo na mifugo

Shahada ya kilimo na mifugo, SUA

Maelezo ya picha hayapo.

Maelezo ya picha hayapo.

IMEPAKULIWA: 08/06/2021

CHANZO: Emmanuel-Mabula-